PRE-MOCK

# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA MJI KIBAHA

# MTIHANI WA KABLA YA UTIMILIFU

# ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

# KIDATO CHA NNE

**MUDA: MASAA 3** **MWAKA:2024**

---

## MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali 11.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na B na maswali mawili (02) katika sehemu C.
3. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
4. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

**SEHEMU "A" (ALAMA 16)**

01. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha andika herufi yake katika kijitabu chako cha kujibia.

i) Ibada gani inaingia katika Faradhi Kifaya katika ibada zifuatazo:- ( )
(A) Hijja (B) Funga (C) Mirathi (D) Swala ya maiti (E) Zakat

ii) Allah (sw) amesema....... "Na ziko kwake funguo za ghaibu hakuna azijuaye ila yeye tu....," Aya hiyo inaeleza kuhusu nguzo gani ya imani ya uislamu. ( )
(A) Kumuamini Allah (sw) (B) kuamini vitabu vya Allah (sw)
(C) Kuamini Qadar ya Allah (sw) (D) Kuamini Mitume ya Allah (sw) (E) Kuamini Malaika wa Allah (sw)

iii) Kuna baadhi ya watu hutoa tafsiri ya dini huku wakihusisha mamlaka ya Allah (sw) na viumbe vyake, kundi hilo lipi kwa mujibu wa makundi ya dini? ( )
(A) Wayahudi (B) Washirikina (C) Watawa (D) Makafiri (E) Waislamu

iv) Katika taaluma ya hadithi, " Mutafaqun ilayhi" ina maana gani? ( )
(A) Imepokewa na Maimamu wote wanne
(B) Imepokelewa na Abu Hanifa na Malik Bin Annas
(C) Imepokelewa na Imamu Bukharin a Muslim.
(D) Imepokelewa na Imamu Muslim na Abu Hanifa.
(E) Imepokelewa na Imamu shafii na Hambar

v) Nabii gani aliyejenga msikiti wa Al Aqsa kwa mara ya kwanza. ( )
(A) Is-haq (as) (B) Il-yaas (as) (C) Suleiman (as)
(D) Idrisa (as) (E) Mussa (as)

vi) " ............ Mwezi wa Ramadhani ambamo (Allah (sw) ameiteremsha Qur'an ...." Allah (sw) anamaanisha ameiteremsha Qur'an kutoka wapi na kuelekea wapi? ( )
(A) Kutoka Lauhul Mahafadh kwenda kwenye uwingu wa dunia.
(B) Kutoka peponi kuja duniani.
(C) Kutoka peponi kwenda Lauhul Mahafudh.
(D) Kutoka kwa Allah (sw) kwenda kwa mtume (saw).
(E) Kutoka Kwa Mtume (saw) kwenda kwa Maswahaba (ra)

vii) Tunajifunza nini katika shahada mbili kama nguzo ya dini ya kiislamu? ( )
(A) Muhammad (saw) ni Mtume wa mwisho.
(B) Hatuwezi kuishi bila kufanikisha wengine.
(C) Ni wajibu kumtii Allah (sw) na Mtume (saw).
(D) Kumuabudu Allah (sw) ipasavyo.
(E) Kulingania uislamu katika jamii.

viii) Ibada yoyote ya kiislamu ina masharti yake, Ni zipi aina mbili za masharti ya swala ya maiti? ( )
(A) Maiti awe ameoshwa na kuvishwa sanda.
(B) Maiti awe Muislamu na aswaliwe na waislamu.

(C) Maiti asiwe mnafiki wala shahidi.
(D) Masharti yanayomuhusu maiti na wale wanaomswalia.
(E) Sehemu ya kuswalia iwe twahara na maiti iwekwe mbele ya wanaoswali.

ix) Ni nini hukumu ya mtu aliyeacha kufunga siku moja kwa makusudi katika mwezi mtukufu wa Ramadhani?
(A) Atatakiwa alipe kadha baada ya mwezi wa Ramadhani.
(B) Hataruhusiwa kuendelea kufunga tena siku zitakazobakia. ( )
(C) Hataweza kulipa hata kama mwaka mzima.
(D) Atatoa kafara ya ngamia mmoja na kumwacha huru mtumwa.
(E) Atafunga miezi miwili mfululizo bila kuacha hata siku moja.

x) Surat Fat-ha ni sura ya kwanza katika msahafu na ni sura pekee ambayo " Bismillahi" ni aya yake ya kwanza. Tunajifunza nini?
(A) Ni lazima kila inaposoma Qur'an uanze na Bismillahi.
(B) Bismillahi ni aya katika sura zote za Qur'an. ( )
(C) Tunapaswa kuanza kila jambo letu kwa kumtanguliza Allah (sw).
(D) Bismillahi ni nguzo katika nguzo za swala.
(E) Mtume (sw) alikuwa hasomi Bismillahi kwa sauti wakati wa swala.

02. Oanisha orodha A na orodha B kasha andika herufi ya jibu sahihi.

| **ORODHA A** | **ORODHA B** |
|---|---|
| i) Ukamilifu wa shahada | A. Shahada moja |
| ii) Kiingilio katika dini ya kiislamu | B. Kutamka shahada |
| iii) Ahadi ya utii kwa Allah (sw) | C. Shahada ya kwanza |
| iv) Ahadi ya utii kwa Mtume (saw) | D. Utawa |
| v) mafungamano ya Allah (sw) na Mtume (saw) | E. Ishara ya shahada |
| vi) Kukanusha shahada kivitendo katika maisha. | F. Shahada ya pili |
| | G. Moyoni, ulimi na matendo ya viungo |

**SEHEMU B (ALAMA 54)**

**JIBU MASWALI YOTE KWA UFUPI KATIKA SEHEMU HII.**

03. Tunasoma Qur'an ili tupate mafunzo yanayotuongoza katika maisha yetu ya kila siku. Waeleze wanajamii kwa ufupi mafunzo sita (06) yanayopatikana katika suratul Asr.

04. Dola yoyote duniani ni lazima iwe na vyanzo vya mapato ili kusaidiana uendeshaji wa dola hiyo kwa kuzingatia kauli hii eleza vyanzo vya mapato katika dola ya kiislamu kipindi cha makhalifa wanne waongofu. Andika hoja sita.

05. Ingawa Mitume walikuwa binadamu lakini walikuwa wana vipawa na sifa za ziada tofauti na watu wengine katika jamii zao. Eleza sifa tatu kwa ufupi.

06. Wanasayansi wa kikafiri wanaamini dini ni matokeo ya hofu ya mwanadamu ndipo akajitengenezea dini, ukiwa msomi wa elimu ya dini ya Kiislamu wabainishie kwanini mwanadamu hawezi kuishi bila ya dini (Toa sababu tatu).

07. Sehemu kubwa ya jamii yetu ya kiislamu na dunia kwa ujumla imekosa furaha na amani kwa sababu ya kukosekana kwa haki na uadilifu kwenye jamii. Elimisha jamii juu ya misingi mitatu ya kusimamisha haki na uadilifu katika jamii.

08. Kwa kutumia nukta tatu (03) bainisha maovu yaliyofanywa na kaumu Lut (as) ambayo yanafanywa na umma wa sasa.

**SEHEMU C (ALAMA 30)**

**JIBU MASWALI MAWILI (02) TU KUTOKA SEHEMU HII.**

09. Wasiokuwa waislamu huona kuwa funga ni kujitesa na kujipa tabu, wewe ukiwa kama mwanafunzi msomi wa elimu ya dini ya kiislamu waelimishe wasiokuwa waislamu kuhusu funga . Tumia hoja tano.

10. " hakika sisi ndio tulioteremsha mawaidha (Qur'an) na kwa hakika sisi ndio tutakayoyalinda" ...(15:9). Kwa mujibu wa aya hii fafanua njia zilizotumika kuhifadhi Qur'an. (Toa hoja tano).

11. Uchambuzi wa hadithi ni moja kati ya taaluma muhimu katika uislamu ili kubaini hadithi sahihi na zisizosahihi ukiwa kama mwanafunzi uliyefundishwa uchambuzi wa hadithi fafanua vigezo vitano vya matini sahihi.

*WABILLAHI TAWFIQ*